## MUSIUZE MASHAMBA PWANI — MOI

**MTUKUFU RAIS MOI amewashauri wananchi wa Pwani waepukane na mtindo wa kuuza mashamba kwani mtindo huo utawaletea majuto kwao na kwa vizazi vyao. Rais Moi alitoa mwito huo wakati akitembelea sehemu za Kusini ya Mombasa huko waa. Alisema Pwani ingali na nafasi kubwa ya kilimo na kutoa mwito kwa wananchi wote wa Pwani kuzidi kufanya bidii katika kazi za mashambani.**

SALAMU ZA MWAKA MPYA:

**Katika salamu zake za mwaka mpya Rais Moi aliwatakia wananchi wote wa Kenya furaha, amani, umoja na upendo kati yao.**

IBADA:

**Katika ibada ya kanisani Mtukufu Rais Moi aliwafahamisha wananchi wa Kenya kwamba utesi kati ya viumbe ni dhihirisho la uhasidi kati ya watu. Alitoa mwito kwa wananchi kusema kweli, kutendeana mema, na kutenda mema kwa taifa.**

**Alisema binaadamu asidanganyike na anasa za ulimwengu na kuleta mateso kwa wengine. Ibada hiyo ilihudhuriwa pia na Mkuu wa sheria Bwana Charles Njonjo, mawaziri katika afisi ya Rais Bwana G. G. Kariuki, na Bw. N. Biwott, Viongozi kadha wengine pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Pwani Bwana Eliud Mahihu. Ibada hiyo iliongozwa na Bishop Mwangombe.**

# JUNGUKUU LAPIKWA PWANI

BARAZA KUU la Waandishi, Washairi na wataalamu wa lugha ya Kiswahili limebuniwa nchini Kenya chini ya uwenyekiti wa Shaha wa mashaha Sheikh Ahmed Sheikh Nabhany, ndugu yetu, Mzee wetu, kiongozi wetu katika utumishi wa lugha ya Kiswahili Kenya.

**na SALEH A. AL-ISMAILLY**

Katika taarifa yake katibu Mkuu wa baraza hilo Bwana Mohamed Kamal Khan ambaye yuwajulikana sana Mvita kwa jina la Maalim Kamal Khan alisema umoja wao utajulikana kwa jina la Jungukuu (Baraza Kuu la Kiswahili), na kwamba baraza hilo lao limeshapewa kibali na Afisi Kuu za Mkuu wa Sheria kwa kuandikishwa rasmi katika serikali.

**MAAFISA WENGINE:**

Maafisa wengine katika umoja huo si wingine isipokuwa wale wale ndugu na wazee wetu: Bwana Mohammed Omar Mazooq (Naibu wa Katibu Mkuu), Bwana Abdulla Barawa (Katibu Mtendaji), Bwana Said Omar Hijazy (Mweka Hazina). Tawi — Nairobi linasimamiwa na mzee wetu Bwana Hassan Mwalimu Mbega.

Maalim Kamal Khan alisema "Mpaka sasa baraza hilo bado halijaunda mpango wa utafiti wa lugha, moja wapo wa mambo yanayotarajiwa kufanywa na vile vile mambo muhimu zaidi ni:

• Kusimamia maendeleo ya Kiswahili kama Lugha ya Taifa na mataifa yanayotumia Kiswahili.

• Kuhifadhi Kiswahili vile inavyohitajika bila kuingizwa maneno ya bandia na upuuzi mwengine usiofaa, kwani Lugha ya Kiswahili ina wenyewe na wapo, wala haikuzuka kutoka binguni na wenyewe ni Waswahili.

• Jungukuu litakuwa likitoa utumishi wa Kitaalamu na kadhalika.

• Jungukuu litatimiza wajibu wake kwa Taifa la Kenya kwa kila njia.

Baraza la Jungukuu litafungua matawi kila sehemu humu nchini.

# Moi karibu Mombasa

*Heko nyingi nazitoa, kwa wazalendo wa Pwani,*
*Kote katika mkoa, Malindi hadi Wundanyi*
*Jinsi walivyo jitoa, kumpokea Rubani*
*Wapwani twakuthamini, Moi karibu Mombasa.*

*Karibu kwetu Mombasa, asubuhi na jioni*
*Tumeupiga msasa, mkoa wote wa pwani*
*Sote tumejitakasa, hakuna kichini chini*
*Wapwani twakuthamini, Moi karibu Mombasa.*

*Hapo aliye na doa, au tuhuma moyoni*
*Hapo wakutupotoa, twakwambia uamini*
*Hakikisho twalitoa, la utwaa na imani*
*Wapwani twakuthamini, Moi karibu Mombasa.*

*Wazee hadi vijana, mkoa huu wapwani*
*Pamoja tumeshikana, kwa undugu na amani*
*Hakuna kamwe fitina, la siasa au dini*
*Wapwani twakuthamini, Moi karibu Mombasa.*

*Chuki na kichini chini, twakuapia "Rubani"*
*Zimekomeshwa zamani, kwenye mkoa wapwani*
*Tembelea mkoani, ujionee machoni*
*Wapwani twakuthamin., Moi karibu Mombasa.*

*Wewe ndie wetu Baba, mbora wa kuamini*
*Mtukufu mahbuba, kipenzi chetu wapwani*
*Tumekungoja kwa huba, Voi mpaka Likoni*
*Wapwani twakuthcmini, Moi karibu Mombasa.*

*Twanyosha yetu mikono, kukusalimu mwandani*
*Kwa sauti ya mungano, wakazi wote wa pwani*
*Twakiri bila kinzano, moi ushike sukani*
*Wapwani twakuthamini, Moi karibu Mombasa.*

*Karibu kwetu Mombasa, mteule wa chamani*
*Mombasa yetu ya sasa, sijaile ya zamani*
*Ya sasa ina anasa, za kiakhiri zamani*
*Wapwani twakuthamini, Moi karibu Mombasa.*

*Wapwani twasema ndiwe, mrithi wa usukani*
*Hatuoni alo jawe, tangu bara hadi pwani*
*Nyayo zako zifwatiwe, mbio tusonge usoni*
*Wapwani twakuthamini, Moi karibu Mombasa.*

*Wapwani twafata nyayo, kwa ukweli na imani*
*Twazifwata mbio mbiyo, hatusoti asilani*
*Nahivyo ndivyo ilivyo, huku mkoa wa pwani*
*Wapwani twakuthamini, Moi karibu Mombasa.*

*Kaditama vaa taji, la kuongoza watwani*
*Ndivyo sote twataraji, ili tuwe furahani*
*Watunzi na waimbaji, wakuzalishe nishani*
*Wapwani twakuthamini, Moi karibu Mombasa.*

**na A. A. KENYA (Jino la Simba)**



• *PICHA YAONESHA msichana wa Kijerumani Bi-Christel Peligris akishangazwa na ujenzi wa kabila la Ki-Orma ndani ya kumbusho la Lamu.* PICHA: SAID ALBURHAN

# Makumbusho yana elimu ya Aushi

**na SAID AL-BURHAN**

WAKATI ULIKUWA ni alasiri. Pahala palikuwa kando ya bahari — mjini Lamu. Ndipo nilipokutana na msichana wa Ujerumani magharibi anatalii katika kisiwa hicho cha Lamu.

Lakini katika maongezi yetu alilalamika kwamba tokea afike katika mji huo hajaona jambo la kumvutia. Hakika utashi wake ni kuona jambo ambalo huko kwao asingeliona maisha yake.

**KUMBUSHO LA LAMU:**

Nami kwa heshima nilimkaribisha katika jumba kuu la makumbusho la Lamu. Siku ya pili yake. Nilikuwa na hakika kwamba ni mahala hapo tu ndipo pangezima kiu ya mtalii huyu.

Kuona tu lile lango la jumba la makumbusho alikiri kwamba ndani ya jumba hilo kuna elimu ya aushi. Sikufanya pupa niliamua kwamba tutalitalii jumba hilo kwa makini hadi yeye mwenyewe atosheke kwamba vyombo vilivyomo ndani ya jumba hilo ni vitu vya historia ya makambali ya Kenya hasa ya mkoa wa Pwani wilaya za Tana River na Lamu.

**ORMA:**

Nilianza kumuonesha mbali mbali na vile utamaduni wao ulivyo. Moja wapo ni utamaduni wa kale sana wa watu wa Kabila la Ki-Orma na ujenzi wa nyumba zao. Alishangaa sana kuona makao hayo ya Orma na kuuliza sana jinsi wanavyoishi humo. Nilipomueleza kwamba akina Orma kila mara huzunguuka huku na huko na mifugo yao kama ilivyokuwa hapo zamani, makao yao yalikuwa ya aina hiyo. Alifurahikiwa mno na nyumba hiyo ya Ki-Orma.

Alipendekeza kuwa ingekuwa jambo la busara sana kwa wananchi wa Kenya wakiwa katika hali ya maendeleo wajenge nyumba za kisasa zenye sura nyumba za Ki-Orma. Nilimuahidi kwamba Kenya inasonga mbele na kwamba haitakuwa ajabu siku moja akirudi Kenya atakuta nyumba ya aina hiyo.

# Sasa wakati wa kazi kuu Manispaa ya Mombasa

KWA MARA nyingine tena baraza la Manispaa ya Mombasa limeundwa tena, sasa tukiwa naye yule yule mpendwa Mayor wa Mji huu Diwani Rajab Sumba, na Naibu wake Diwani Mwidani. Haya yalikuwa ni matakwa ya watu wa Mombasa, na kwamba ushindi wa Diwani Sumba na Diwani Mwidani ni imani ya watu wa Mombasa ILIYO—DHIHIRIKA KWA VITENDO.

**na SALEH A. AL-ISMAILLY**

Maongozi ya Nyayo ya Mtukufu Rais Moi, ndio muanga unaongoza kila kitu katika hali ya maisha ya watu wote wa Pwani. Ushindi huu ni ushindi vile Nyayo zinavyofuatwa Mombasa.

Umoja wetu, upendo, na furaha, pamoja na maendeleo ni msingi wa maongozi na lengo la Rais Moi kwa watu wote wa Kenya. Tukumbuke mahasidi wa Kenya wa aina nyingi hawafurahi kuona haya yote. Hupendelea kupata wao tu, na kuusahau Umma wa Kenya. Msimamo wetu ni wa imani kamili kabisa kwa Rais Moi na serikali yake, na hatutarudi nyuma kamwe isipokuwa kuzidi kusonga mbele.

**MAAFISA**

Baraza la Mji wa Mombasa sasa lina wajibu na jukumu kubwa kutekeleza mengi. Lakini utumishi huo utakuwa si ndoto ikiwa wananchi wote watazidi kushikamana na Mayor, madiwani wote na maafisa wote wa Manispaa katika kutatua matatizo ya Mombasa. Hivi juzi tu Mkuu wetu wa wilaya Bw. F. Cherogony alitaja tatizo la upungufu wa Madarasa katika vidato vya kwanza katika shule za msingi Mombasa. Wakati wa maneno umekwisha lakini tukumbuke kwamba kupiga kura tu haitoshi ni lazima kila mmoja wetu, kutwaa sehemu yake.

Mabaraza ya wazee yakishirikiana na baraza la manispaa na afisi ya elimu ya Manispaa na wananchi wote, yataweza kutekeleza mengi. Wenzetu huko Amerika wameweza kwenda mwezini kwa umoja wao na juhudi zao, nasi kwa umoja wetu, tukiwa na nia moja, tutashinda kwa mengi.

Nia zetu ziwe moja, kwani umoja ni nguvu. Lile la kufanywa kwa haraka. Ni juu ya baraza la Manispaa kutwambia, kwa hivyo raia wapo tayari hasa kwa vile madarasa yatakikana kwa haraka sana katika mwaka huu huu mpya ili watoto wetu, ndugu zetu wasikose nafasi.


SALE KUBWA YA MWAKA
inaendelea katika duka la
Shankar Electronics
Barabara ya Moi Avenue, Mombasa
*Utapata shati moja bure kwa kununua kila radio moja*
*Bei za chini sana*


## Coastweek ** JEMBE

SWAHILI CROSSWORD NO. 59


*KWENDA KULIA:*

1. Aina ya mkate wa mayai
7. Kurukia, kupandia kama kurukia gari
8. Namna ya mdudu
9. Kuingilia kwa nguvu
10. Jina la Kijaluo
12. Weka sehemu mbali mbali
14. Kiungo cha chakula
16. Ndani kwa Kimombo
17. Jina la kiume
19. Vyombo vya bahari

*KWENDA CHINI:*

1. Kiswahili
2. Chumvi
3. Mfalme wa mwituni
4. Nusu ya Dada
5. Atolewa maziwa
6. Kiwanda cha kuundia motakaa au vyombo vya mitambo
11. Hutokana na miti
13. Juma
15. Toa machozi
17. Kama, mfano
18. "Az" haibadiliki


JEMBE
UNGA SAFI NO. 1
WA MAHINDI

JINA. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

SANDUKU LA POSTA. . . . . . . . . . . . . . . .

. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 57:**

[1] Mishi Arif Hassan M., Sanduku la Posta 90462, Msa,

[2] Abdulhamid A. Batog, Sanduku la Posta 80074, Msa,

[3] M. Muriuki Jadiel, Sanduku la Posta 84126, Msa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*

**MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 57:**

**KWENDA KULIA:**

1. BEMBEA, 4. UA, 6. IS, 8. NGAMANI, 10. MGALA, 12. DIRISHA, 13. RIA, 15. IAA, 16. ANZA, 18. LA, 20. UITEME, 22. JA, 23. LA.

**KWENDA CHINI:**

1. BENDERA, 2. MAANDAZI, 3. AINGIA, 5. AKWAA, 7. SIASA, 9. AMRI, 11. LH, 14. INUA, 17. ATI, 19. AFA, 21. MO.

### Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindi watatu wa kwanza kila mmoja atapatiwa T-shirt moja ya Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LTD* pamoja na ATTA LTD Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, *COASTWEEK* Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya, siku ya Alhamisi tarehe 10.1.80 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.